Kadi ya Ripoti ya
Mkoa wa Manitoba

# Taarifa kwa Wazazi

DARASA LA 9 MPAKA 12



Manitoba

*Elimu ya Manitoba imezindua kadi ya ripoti ya kimkoa ya lazima kwa wanafunzi wa taaluma zote kuanzia mwaka wa shule 2013/2014.*

# Kwa Ujumla

### Kwa nini kuna kadi mpya ya ripoti?

Serikali ya Manitoba imezindua kadi mpya ya ripoti ya kimkoa kuboresha elimu Manitoba na kujenga ushirikiano mzuri kati ya wanafunzi, walimu wao na wazazi.

Hapo nyuma, kadi ya ripoti ilikuwa tofauti kwa kila darasa na, mifano mingine, kwa baadhi ya shule ndani ya madarasa sawa. Kadi mpya ya ripoti ya kimkoa itahakikisha kwamba wazazi wanapata taarifa sahihi mara kwa mara za namna watoto wao wanajifunza, hatua wanazojitahidi, ni hatua gani zitasaidia zaidi kujifunza na nini wanaweza kufanya kuwasaidia.

### Je, kadi ya ripoti itakuwa rahisi kuielewa?

Kadi ya ripoti inaandikwa kwa lugha nyepesi. Inakuambia uwezo wa mtoto wako na wapi mtoto wako anahitaji msaada. Kama una maswali kuhusu kadi ya ripoti, unaweza kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako.

### Je, kadi ya ripoti ya taaluma ni sawa kwa madarasa yote?

Kuna mitindo mitatu ya kadi ya ripoti: moja ya Darasa la 1 mpaka 6, ya Darasa la 7 na 8 na nyingine ya Darasa la 9 mpaka la 12.

### Je, kutakuwa na maoni ya mwalimu kwenye kadi ya ripoti?

Ndiyo. Walimu wataandika maoni kuhusu kazi na tabia ya mtoto wako shuleni. Maoni yatakusaidia kutambua ni nini mtoto wako anafanya na msaada anahitaji wa kujifunza.

### Je, mtoto wangu anatathminiwa vipi?

Alama anazopata za kielemu zinaonesha jinsi mwanafunzi anavyofikia malengo ya mwongozo wa mtaala wa kusoma. Hii inajulikana kama vigezo vya alama vinavyoangaliwa. Alama anazopata mtoto wako haziwekwi kwa kulinganisha na za wanafunzi wengine. Mambo kama mtazamo, juhudi na tabia zinaripotiwa kando na mafanikio ya kielimu. Huku ikieleweka kwamba vitu hivi vinaweza kuathiri matokeo ya kielimu na hivyo alama, kuviripoti kando husaidia kumpa mzazi habari ya ziada kuhusu uwezo wa mtoto wake na maeneo anafaa kuboresha.

Walimu hutoa njia nyingi za kuonesha ujuzi wao na kuelewa somo. Alama anazopata kwa ujumla zina akisi matokeo ya sasa na yanayoendelea ya kitaaluma. Kwa mfano, hii ina maana kwamba alama ya chini ya zoezi la mwanzo wa kufungua shule linaweza lisitiliwe mkazo katika kuamua alama za mtoto wako mwisho wa muhula kama baadaye alionesha mfululizo wa kujitahidi wa kuelewa zaidi au kupata ujuzi zaidi katika eneo hilo.

### Ni kwa namna gani alama zitaripotiwa?

Alama za wanafunzi zinaripotiwa kwa kutumia asilimia.

### Mtoto wangu anaweza kufeli kozi?

Ndiyo. Darasa la 9 mpaka 12 (shule ya sekondari), alama zinapatiwa kulingana na ushahidi unaoonekana wa kujifunza uliowekwa na mitaala ya mkoa. Alama za mwisho za chini ya asilimia 50% zinaonesha kwamba mwanafunzi hakufaulu vizuri katika ujuzi na maarifa ya kozi.



### Ni lini kadi ya ripoti itatumwa nyumbani?

Kwa muhula wa shule, kadi za ripoti zinatumwa nyumbani mara mbili kwa muhula. Kama si kwa muhula wa shule, zinatumwa nyumbani wakati wa kipupwe, masika na mwisho wa mwaka.

### Je, nitapata taarifa kutoka kwa walimu wakati mwingine?

Ndiyo. Kadi ya ripoti ni njia pekee ya kuwasiliana na wazazi. Njia nyingine ni pamoja na simu, barua pepe, ripoti ya maendeleo isiyo rasmi, mkutano wa wazazi na walimu, kongamano la wanafunzi na taarifa za habari za shule.

*Katika waraka huu, neno wazazi lina maanisha wazazi au walezi.*

### Nifanye nini kama nina wasiwasi na utendaji wa mtoto wangu shuleni?

Ongea na mwalimu wa mtoto wako. Itakuwa ni jambo la busara kuorodhesha maeneo ambayo mtoto wako anapata shida. Muulize mwalimu ni namna gani mnaweza kufanyakazi pamoja kumsaidia mtoto wako.

# Programu za mwanafunzi

*Programming* ya mtoto wako inamaanisha kama mtoto wako anafuata mtaala kwa ngazi, au ngazi ya daraja la mitaala mahususi inayoonesha mahitaji yake ya kujifunza.

Kwa Darasa la 9 na 12 (shule ya upili), kozi zinatumia mfumo wa namba tatu. Namba tatu (mf., 20F – "F", kwenye mfano huu) inarejea kwenye aina ya programu mtoto wako anafuata. Kama mtoto wako anafuata alama za mtaala za darasa kwenye somo, kadi yake ya ripoti itatumia moja ya alama zifuatazo:

F (Foundation), S (Specialized) or G (General).

Kama mtoto wako *hafuati* alama za ngazi ya mtaala katika somo, kadi ya ripoti itaonesha ni ipi kati ya programu tatu zifuatazo zitumike (na alama za herufi zinazoambatana)



## 1. M programming

"M" inarejea programu inayorekebishwa inayohitajika kwa sababu ya ulemavu wa akili (ufahamu) ulemavu. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inarejea malengo ya kujifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi, na malengo hayo yanaelezewa wazi katika mpango binafsi wa mwanafunzi (IEP).

## 2. E programming

"E" inarejerea kwenye Kiingereza kama nyongeza ya programming ya lugha (EAL). Mwanafunzi wa kwenye hatua ya kwanza ya kujifunza Kiingereza kama lugha ya ziada inalenga katika kujifunza Kiingereza katika eneo la somo hilo. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inazingatia kwenye usawa wa lugha na malengo ya eneo la somo analojifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi kwa kiwango cha lugha anayofahamu. Malengo hayo yameelezewa vizuri kwenye mpango wa elimu wa mwanafunzi wa EAL.

## 3. L programming

"L" inarejelea kwenye programu ya kujifunza Kiingereza, na inatumika kwenye programu ya *Français* na programu ya kujifunza Kifaransa kwenye Darasa la 9 na 12. Mwanafunzi ambaye anahitaji msaada zaidi wa kuendeleza ujuzi wa lugha ya Kifaransa anatakiwa kufuata mtaala wa mkoa na kuzingatia kujifunza Kifaransa katika muktadha wa eneo hilo la somo. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inazingatia kwenye usawa wa lugha na malengo ya eneo la somo analojifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi kwa kiwango cha lugha anayofahamu. Malengo hayo yameelezewa vizuri kwenye mpango wa elimu wa kujifunza Kifaransa.

Kwenye mfano hapo chini, unaweza kuona ambapo ni aina gani ya programu inaoneshwa kwenye mduara mwekundu. Katika kesi hiyo, mwanafunzi anafuata mabadiliko ya programu ("M") kwenye somo la hisabati.

| | Attendance and Achievement | | | | | | | | Learning Behaviours | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Term 1 | | | Term 2 | | | Final | | Term 1 | | | Term 2 | | |
| | Lates | Absences | Grade | Lates (Total) | Absences (Total) | Grade | Final exam | Final grade | Personal management skills | Active participation in learning | Social responsibility | Personal management skills | Active participation in learning | Social responsibility |
| Semester:<br>Teacher:<br>Credit Value:<br>Credits Earned: | Course: **Mathematics 10M** | | | | | | | | | | | | | |
| | | | % | | | % | % | % | | | | | | |
| | Comments: | | | | | | | | ❑ IEP (behaviours) | | | | | |

# Mafanikio ya kielimu ya matarajio ya mkoa

Asilimia ya alama ya kipimo inatumika kwenye kadi ya ripoti ya wanafunzi kuonesha alama kwa ujumla kwa kila somo analochukua. Chati hapa chini inaonesha jinsi alama ya asilimia inahusiana na mafanikio ya kielimu katika somo hilo, ikiwa ni pamoja na namba nyingine zinazotumika. Kumbuka kwa Darasa la 11 na 12 Elimu ya Kimwili / kozi ya Elimu ya Afya, alama kwa asilimia hazitumiki. Badala yake, Codi **CO** na **IN**, imeelezewa hapo chini, zinatumika kwenye kadi ya ripoti.



| Academic Achievement of Provincial Expectations | Percentage Grade |
|---|---|
| Very good to excellent understanding and application of concepts and skills | **80% to 100%** |
| Good understanding and application of concepts and skills | **70% to 79%** |
| Basic understanding and application of concepts and skills | **60% to 69%** |
| Limited understanding and application of concepts and skills; see teacher comments | **50% to 59%** |
| Does not yet demonstrate the required understanding and application of concepts and skills; students with a final grade of less than 50% are not granted course credit; see teacher comments | **Less than 50%** |
| **Additional Codes** | |
| **Course Complete:** Final passing grade for courses using CO/IN for grades, e.g., Grades 11 and 12 Physical Education/Health Education. | **CO** |
| **Course Incomplete:** Final grade showing insufficient evidence of learning for courses using CO/IN for grades, e.g., Grades 11 and 12 Physical Education/Health Education. May also be used in other courses but not as a final grade. | **IN** |
| No exam applies | **NE** |
| No mark for the school-based final exam or provincial test, where applicable | **NM** |

Mfano ufuatao unaonesha mwanafunzi wa Darasa la 10 anayechukua Sayansi na alama za kawaida za programu ya mtaala wa alama za kipimo. Pia inaonesha mienendo mitatu ya kujifunza, ambayo imeelezewa sehemu ya hapo chini. Inajumuisha mtihani wa mwisho wenye asilimia 20% ya alama za mwisho.

| | **Attendance and Achievement** | | | | | | | | **Learning Behaviours** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Term 1** | | | **Term 2** | | | **Final** | | **Term 1** | | | **Term 2** | | |
| | Lates | Absences | Grade | Lates (Total) | Absences (Total) | Grade | Final exam | Final grade | Personal management skills | Active participation in learning | Social responsibility | Personal management skills | Active participation in learning | Social responsibility |
| Semester: 1 | Course: **Science 20F** | | | | | | | | | | | | | |
| Teacher: Ms Osmand | 2 | 1 | 70% | 3 | 1 | 75% | 80% | 76% | C | U | S | U | S | C |
| Credit Value: 1 | Comments: | | | | | | | | ❑ IEP (behaviours) | | | | | |
| Credits Earned: 1 | | | | | | | | | | | | | | |

# Kuhitimu shule ya sekondari

Katika Darasa la 9-12 (shule ya sekondari), wanafunzi wanaweza kupata alama wanapomaliza kwa kila somo wanalochukua, watakapofaulu kwa zaidi ya asilimia 50% (au zaidi).

Taarifa kwa wazazi kuhusu mahitaji ya kuhitimu zinapatikana mtandaoni kwenye:

**www.edu.gov.mb.ca/k12/policy/grad_require.html**

Ni muhimu wewe na mtoto wako kuhakikisha alama za mtoto wako zinamruhusu kuhitimu, na zinaendana na mpango wa mtoto wako baada ya kuhitimu. Kadi ya ripoti ina jedwali linaloonesha maendeleo anayopata mtoto wako wakati anakaribia kuhitimu. Kama utakuwa na chochote kuhusu hili, wasiliana na shule ya mtoto wako.


# Tabia za kujifunza

Pamoja na kuripoti mafanikio ya kitaaluma, kadi ya ripoti inaonesha jitihada za mtoto wako na tabia darasani, zinazoripotiwa chini ya "Mienendo ya Kujifunza," kama ilivyoelezwa katika mfano hapo mwanzo na hapo chini. Sanduku la IEP katika sehemu hii litatumika kama mtoto wako ana mpango binafsi wenye malengo yanayohusiana na mienendo ya kujifunza.

| Learning Behaviours | |
|---|---|
| **Scale** | **C**: Consistently – almost all or all of the time<br>**U**: Usually – more than half of the time<br>**S**: Sometimes – less than half of the time<br>**R**: Rarely – almost never or never |
| **Personal management skills** | Uses class time effectively; works independently; completes homework and assignments on time |
| **Active participation in learning** | Participates in class activities; self assesses; sets learning goals |
| **Social responsibility** | Works well with others; resolves conflicts appropriately; respects self, others and the environment; contributes in a positive way to communities |

Mienendo ya kujifunza haijajumuishwa moja kwa moja katika alama za mwanafunzi, lakini zinaweza kuathiri matokeo yao ya kitaaluma. Maendeleo chanya ya miendendo ya kujifunza yanaweza kusababisha mafanikio ya baadaye ya wanafunzi wakati wanaendelea na maisha yao kote ndani na nje ya shule. Kama wanafunzi wanafanya kazi kwa kujitegemea, huchukua hatua na kuheshimu maadili ya darasa, stadi hizi zinakwenda sehemu nyingine nyingi za maisha yao.

Kwa wanafunzi katika Programu ya Kuzamishwa kwenye Kifaransa, pia kuna mienendo ya kujifunza kuhusu ushiriki wa wanafunzi katika kutumia Kifaransa.



# Kwa taarifa zaidi

Tembelea tovuti ya Elimu ya Manitoba kwa taarifa zaidi kuhusu

- kile mtoto wako anajifunza kwenye **maeneo mbalimbali ya masomo:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/cur/parents/ (Programu ya Kiingereza)
  www.edu.gov.mb.ca/k12/cur/parents/fr_imm/ (Programu ya Kujifunza Kifaransa)
  www.edu.gov.mb.ca/m12/progetu/parents/ (Programu ya *Français*)
- sera na miongozo ya **tathmini ya mwanafunzi:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/
- **Kadi ya Ripoti ya Taaluma:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/report_cards/index.html

# Maoni yako yanakaribishwa

Uwe mzazi au mlezi, mwalimu, mwanafunzi au mwanajamii, maoni yako kwenye kadi ya ripoti mpya ni ya muhimu. Kwa ujumla, umeona hii kadi ya ripoti kuwa ya kuaeleweka na ya kukupasha taarifa? Kuna sehemu ya ripoti ambayo inaweza kuboreshwa zaidi?

Kama unataka kutoa maoni, tafadhali tuma barua kwenye anwani hapo chini au tembelea tovuti iliyotolewa hapo juu na jaza fomu na kutuma maoni yako sehemu ya kutoa maoni.

| Maoni kwenye Barua | Maoni kwenye Mtandao |
|---|---|
| *Provincial Report Card Feedback*<br>Manitoba Education<br>1567 Dublin Avenue<br>Winnipeg MB  R3E 3J5 | www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/report_cards/feedback.html |

